TAARIFA YA MAENDELEO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI

Utanguliza:

Halmashauri ya Wilaya ya Ngara ina jumla ya shule 29, kati ya hizo 23 ni za serikali na 6 ni za binafsi. Aidha miongoni mwa hizo kuna shule 5 za kidato cha tano na sita zikiwemo 4 za serikali na 1 ni ya binafsi hivyo kutimiza azima ya Serikali ya kila tarafa kuwa na shule ya kidato cha tano na sita. Halmashauri ya Wilaya ina jumla ya walimu 470 kati ya hao walimu wanaofundisha masomo ya sanaa ni 395 na wanaofundisha masomo ya hisabati na sayansi ni 75. Jukumu kubwa la idara ya Elimu Sekondari ni kuhakikisha kuwa vijana wote wanaojiunga na masomo ya Sekondari wanahitimu na kufaulu kwenye mitihani yao ya mwisho.

Hali ya Taaluma

1. **Matokeo ya kidato cha nne (CSEE) 2015 hadi 2017**

Matokeo ya mitihani ya taifa ya kidato cha nne (CSEE) miaka mitatu mfululizo yaani 2015, 2016 na 2017 yanaonesha kuwa hali ya taaluma kwa shule za sekondari katika Halmashauri ya Wilaya ya Ngara inaridhisha. Jedwali na 1 hapa chini linaonesha ufaulu kwa madaraja ya watahiniwa wa kidato cha nne kwa miaka ya 2015, 2016 and 2017;

Jedwali na.1

MWAKA	MADARAJA					% UFAULU
	I	II	III	IV	0	
2015	31	208	286	717	602	**67%**
2016	29	147	278	629	219	**83%**
2017	40	174	297	688	312	**79%**

Jedwali na.2 hapa chini linaonesha Halmashauri ya Wilaya ya Ngara imeshika nafasi ya ngapi katika mkoa wa Kagera katika kipindi cha 2015 – 2017

Jedwali na.2

MWAKA	NAFASI KIMKOA	NAFASI KITAIFA	% YA UFAULU
2015	4 kati ya 8	57 kati ya 178	69
2016	4 kati ya 8	26 kati ya 178	83
2017	3 kati ya 8	46 kati ya 178	79.3

Matokeo ya kidato cha Sita (ACSEE) 2016 hadi 2018

Matokeo ya kidato cha sita ya Taifa shule zote zenye kidato cha sita ikiwa shule 1 inamilikiwa na Kanisa Katoliki na shule 4 zinamilikiwa na Serikali zote zinafaulu kwa asilimia 100. Rejea jedwali na.3 lifuatalo:-

Jedwali na.3

MWAKA	MADARAJA							
	I	II	III	IV	I-IV	%	0	%
2016	54	137	112	4	307	100	0	0
2017	68	214	116	1	399	100	0	0
2018	81	369	143	5	598	100	0	0

2. Matokeo ya kidato cha sita ya mitihani ya Taifa tangu 2016 hadi 2018 ya kila shule

Jedwali na.4 Matokeo ya Taifa ya kidato cha sita Mwaka 2016

NA	JINA LA SHULE	MADARAJA						NAFASI KIWILAYA	NAFASI KIMKOA	NAFASI KITAIFA
		I				I-IV	%			
1	LUKOLE	21	50	35	0	106	100	1/4	3/20	90/423
2	MUYENZI	5	16	13	0	34	100	2/4	4/6	17/117
3	RULENGE	12	11	1	0	24	100	3/4	9/20	122/423
4	KABANGA	16	60	63	4	143	100	4/4	12/20	223/423
	TOTAL	**54**	**137**	**112**	**4**	**307**	**100**			

Jedwali na.5 Matokeo ya Taifa ya kidato cha sita Mwaka 2017

NA	JINA LA SHULE	MADARAJA						NAFASI KIWILAYA	NAFASI KIMKOA	NAFASI KITAIFA
		I	II	III	VI	I-IV	%			
1	MUYENZI	5	16	13	0	34	100	1/4	4/21	81/423
2	RULENGE	9	10	6	0	25	100	2/4	4/9	31/146
3	LUKOLE	28	125	50	1	204	100	3/4	7/21	130/449
4	KABANGA	26	63	47	0	136	100	4/4	9/21	114/449
	TOTAL	**68**	**214**	**116**	**1**	**399**	**100**			

Jedwali na.6 Matokeo ya Taifa ya kidato cha sita Mwaka 2018

NA	JINA LA SHULE	MADARAJA						NAFASI KIWILAYA	NAFASI KIMKOA	NAFASI KITAIFA
		I	II	III	IV	I-IV	%			
1	RULENGE	13	25	3	0	41	100	1/5	2/28	31/543
2	LUKOLE	42	195	59	0	296	100	2/5	5/28	89/543
3	MUYENZI	3	50	11	0	64	100	3/5	6/28	99/543
4	KABANGA	20	73	52	4	149	100	4/5	10/28	195/543
5	MURUSAGAMBA	3	26	18	1	48	100	5/5	13/28	248/543
	TOTAL	**81**	**369**	**143**	**5**	**598**	**100**			

MAPOKEZI YA FEDHA ELIMU BILA MALIPO

Halmashauri kupitia akaunti za shule kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ilipokea kiasi cha Tsh.1,005,429,684.00 ikiwa ni fedha ya fidia ya ada, ruzuku ya uendeshaji,ruzuku ya chakula kwa shule za bweni na posho ya madaraka kwa wakuu wa shule 23 zinazomilikiwa na serikali.

NA	KASMA	ROBO 1	ROBO 2	ROBO 3	ROBO 4	JUMLA
1	FIDIA YA ADA	38,123,705.00	38,137,945.00	38,137,945.00	38,137,945.00	152,537,540.00
2	RUZUKU YA UENDESHAJI(CAPITATION)	27,250,709.00	28,066,756.00	28,028,215.00	28,028,215.00	111,373,895.00
3	RUZUKU YA CHAKULA(SCHOOL MEALS)	149,861,673.00	176,730,213.00	173,204,330.00	172,722,033.00	672,518,249.00
4	POSHO YA MADARAKA	17,250,000.00	17,250,000.00	17,250,000.00	17,250,000.00	69,000,000.00
JUMLA		32,486,087.0	60,184,914.00	256,620,490.00	256,138,193.00	1,005,429,684.00

UTEKELEZA WA MIRADI KWA MWAKA 2017/2018

Halmashauri ya wilaya kupitia idara ya Elimu Sekondari kwa mwaka ulioishia Juni 2018 ilitekeleza miradi ya ujenzi wa miundombinu ya bweni moja lenye thamani ya **Tsh.191,618,752.16** lenye uwezo wa kubeba wanafunzi 112 katika shule ya sekondari Muyenzi kwa ufadhili wa Mamlaka ya elimu Tanzania (TEA). Vilevile Halmashauri inaendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa madarasa 4 katika shule za Rusumo B darasa 1, Ngara 1 na Nyamiaga madara 2 na kukamilisha maabara 22 za sayansi katika shule za Shunga,Rusumo,Kanazi, Kibimba,Ndomba, Mugoma na Bukiriro kwa **Tsh.212,042,140.94** chini ya ufadhili wa Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo (EP4R).

USAJILI WA WANAFUNZI MWAKA 2018

Usajili wa wanafunzi wa kidato cha kwanza waka 2018

Halmashauri ya Wilaya ya Ngara ilipangiwa wanafunzi kidato cha kwanza **3813** kwa mwaka 2018 ikiwa sawa na asilimia **100** ya wanafunzi wote **3813** waliohitimu darasa la saba kwa mwaka 2018 kujiunga na shule za kutwa. Kati ya wanafunzi waliochaguliwa, walioripoti ni wanafunzi **3564** Sawa na **93%.**

Usajili wa wanafunzi wa kidato cha tano mwaka 2018

Halmashauri ya Wilaya ya Ngara ilipangiwa na OR-TAMISEMI wanafunzi kidato cha tano **839** kwa mwaka 2018. Kati ya wanafunzi waliochaguliwa, walioripoti ni wanafunzi **664** Sawa na **79%** hadi sasa.

MAFANIKIO

Kuna baadhi ya mafanikio tuliyofikia;

i. Ufaulu wa wanafunzi kwa mtihani wa Taifa wa kidato cha nne na sita kuongezeka kwa kipindi cha miaka mitatu.
ii. Kata zote zina shule za sekondari isipokuwa kata ya Nyamagoma ambayo ni kata mpya.

iii. Kila Tarafa ina shule ya kidato cha tano na cha sita.
iv. Kila shule kujifunza masomo ya sayansi kwa vitendo kutokana na upatikanaji wa vifaa na madawa ya maabara yanayotokana na fedha ya ruzuku ya uendeshaji.
v. Kukamilisha maabara 46 kati ya maabara 72 zinazohitajika wilaya nzima ambazo ni sawa na asilimia 64.

CHANGAMOTO

Pamoja na mafakio tajwa Idara ya Elimu Sekondari inaendelea kukabiliana na changamoto kadhaa;

i. Utoro wa reja reja kwa baadhi ya wanafunzi ambao huathiri ujifunzaji.
ii. Umbali mrefu wa makazi ya wanafunzi na walimu kutoka/kwenda shuleni.
iii. Baadhi ya wanafunzi wanaishi katika mazingira yanayoathiri ujifunzaji wao.
iv. Upungufu mkubwa wa walimu wa Hisabati na Sayansi
v. Upungufu wa miundombinu ya nyumba za walimu,vyoo vya wanafunzi, vyumba vya madarasa na majengo ya utawala.

Mikakati ya Kuboresha Taaluma

Baadhi ya mikakati ya kuboresha ufaulu wa wanafunzi katika mwaka 2018;

i. Wakuu wa shule na walimu wameelekezwa kudhibiti utoro wa reja reja kwa wanafunzi kwa kusimamia mahudhurio ya wanafunzi na kutoa ushauri nasihi.
ii. Idara ya Elimu Sekondari kwa kushirikiana na Wathibiti Ubora wa Elimu wa wilaya wanafanya ufuatiliaji wa mara kwa mara shuleni.
iii. Kujenga daharia/hostel katika shule za kutwa kwa kuishirikisha na kuihamasisha jamii kuona umuhimu wa daharia hizo.
iv. Kuweka kambi za masomo kwa madarasa ya mitihani ya Taifa Mitihani inapokaribia kufanyika.
v. Wakuu wa shule na walimu wa taaluma wanahimizwa kusimamia utekelezaji wa maelekezo ya Afisaelimu Mkoa ya kutoa mazoezi yenye ubora kila siku za masomo hasa kwa wanafunzi wa kidato cha II na cha IV.
vi. Kufanya mitihani ya utimilifu (Mock) ya Wilaya na Mkoa pamoja na mitihanin ya ujirani mwema.